



**TRANSLATORS**  
WITHOUT BORDERS

SWAHILI

Kiwango na ubora wa utoaji wa habari kuhusu  
**ugonjwa wa corona**



utafti iliyo endeshwa na shirika Translators without Borders (TWB)  
jimboni Kivu ya kaskazini, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo

## Matokeo ya kwanza

Matokeo ya kwanza inayo husu hii utafiti inapatikana hapo chini. Hii matokeo ina ambatana na mazungumuzo iliyo fanyika kati ya mwisho wa mwezi wa 8 na mwisho wa mwezi wa 11 mwaka 2020 na iliyo shirikisha washiriki 45 katika jimbo ya Kivu ya kaskazani (Beni, Butembo, Goma, Mabalako). Ni muhimu kujua kwamba hii matokeo haiambatani na maoni ya watu wote wa jimbo ya Kivu ya kaskazini au wa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Lakini, hii matokeo inaweza kusaidia mashirika yasiyo kuwa ya serkali (ONG) kuelewa wasiwasi na mahitaji ya habari kuhusu ugonjwa wa corona katika jimbo ya Kivu ya kaskazini. Hii matokeo inaweza pia kuongoza mashirika (ONG) katika kuanda na kuboresha utoaji wao wa habari kuhusu ugonjwa wa corona.

### Washiriki wanasema nini kuhusu ugonjwa wa corona?

- Karibu washiriki wote walizungumuza juu ya vinyume vya ugonjwa wa corona katika maisha yao ya kila siku. Wanataja shida za kiuchumi, viziwi katika matembezi, kufungwa kwa masomo na makanisa, mabadiliko katika namna ya kuwasiliana na wengine kufuatana na hatua za kujikinga zenye zilianzishwa.
- Washiriki walisema wanapokea habari mara mingi kupitia radio na television. Washiriki wengi wanasema kwamba habari ziko rahisi kueleweka kwa sababu zinatangazwa mu luga yenye wanaelewa muzuri.
- Washiriki wanasema kwamba jamii haijali sana kuhusu ugonjwa wa corona na kwamba watu wachache njo wanaendelea kuheshimu hatua za kujikinga. Hizi tabia zinaweza tokana na mambo mengi kama vile upungufu wa inchi wa kutoa habari kuhusu ugonjwa wa corona, kushuka kwa hesabu ya watu waliyo ambukizwa, lakini pia watu kuchoka na hii janga ya magonjwa na kutoheshimu hatua za kujikinga kama vile kuvala mask (cache nez) au kueshima umbali na watu wengine.
- Washiriki wanagundua ya kwamba kuna mashaka ndani ya jamii kuhusu kuwepo kwa virusi (ugonjwa) mu Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Virusi (ugonjwa) inaweza kuonekana kama «biashara», silaha ya kisiasa au njia ya kuumiza / kusumbua watu. Hii hali inaweza endelea kwa kutokosa uuwazi wa kutosha katika namna ya kukamata hatua za kujikinga kulingana na ma eneo na kutokuheshimu hatua za kujikinga zilizo kamatawa na wakubwa wa inchi.
- Washiriki wengine wanaonekana kuwa na wasiwasi juu ya chanjo ya corona yenye inaweza kupaniwa wakisema kwamba watafanya jaribio ku mwili zabo na kwamba ilitengenezwa juu ya kuwatesa.

### Ni habari na ma swali gani washiriki wanatamani kujua kuhusu ugonjwa wa corona?

- Washiriki wengi wanasema wana hitaji kujua habari zaidi kuhusu ugonjwa wa corona. Mada ambayo iliombwa kuzungumuziwa inahusu: matunzo na kupona, tofauti kati ya virusi ya corona na magonjwa ingine, njia za kuambukiza ugonjwa, utumiaji wa mask (cache nez), chanzo ya ugonjwa wa corona, wagonjwa wasiyo oneshwa alama za ugonjwa, kuambukizwa tena, kipimo cha ugonjwa wa corona. Washiriki wengine wangependa pia kupokea habari juu ya hali ya magonjwa katika inchi na ndani ya jimbo zao na kusikia ushuhuda ya watu waliyo pona ugonjwa wa corona.



- Washiriki wengi wanakosa habari za uhakika na zilizo chunguzwa kuhusu chanjo ya corona yenye inaweza kupaniwa (usalama wa chanjo, maendeleo katika kutengeneza chanjo, kupatikana kwa chanjo mu siku zijazo).

### Washiriki wanapendekeza nini kwa ajili ya kuboresha upashaji wa habari kuhusu ugonjwa wa corona?

- Uhimizaji zaidi kuhusu ugonjwa wa corona ndani ya jamii na hasa vijijini. Uhimizaji unapashwa fanyika zaidi kupitia radio na uso kwa uso na mu luga zote juu ya kuhakikisha kama kila mtu ndani ya jamii anaelewa. Washiriki wengine pia wanapendekeza kugabula ma kartasi yenye kuandikwa ako habari (brochures) ao kubandika ma affiches kama vile ilikuwaka wakati wa Ebola.
- Washiriki wangependa kupata fursa ya kuuliza ma swali kuhusu ugonjwa wa corona na kupokea ma jibu mara moja, kwa mfano kupitia vipindi vya radio ambapo watu wanazungumuza kwa kubadilishana mawazo ao kupitia uhimizaji wa uso kwa uso. Wanamemba wa CAC walipendekezwa kuwa kama watu wanao faa kwa ajili ya kufanya uhimizaji wa uso kwa uso.

## Ma swali na ma jibu kuhusu hii utafiti

### Hii utafiti inahusu nini?

Hii utafiti inahusu ugonjwa wa COVID-19 / ugonjwa wa aina ya virusi ya corona na habari ambayo watu wanapokea kuhusu hii virusi. Ina shaba ya kuelewa kama habari kuhusu ugonjwa wa corona ni muhimu kwa watu, kama wanapokeaka hizi habari na wala kama hawazipokeyi.

### Nini njo lengo ya hii utafiti?

Kupitia hii utafiti, tunataka kuboresha habari kuhusu ugonjwa wa corona. Tutachangia matokeo ya hii utafiti na mashirika zingine kwa ajili waweze kuendelea kuboresha upashaji wao wa habari na kuhakikisha kama hizo habari zinajibu ma swali ya watu.

### Ni nani anaye shiriki katika hii utafiti?

Wachunguzi (enqueteurs) wetu wana hojiana na watu karibu 45 katika jimbo ya Kivu ya kaskazini (pa Beni, Butembo, Goma na Mabalako). Mahojiano inafanyika mu luga mingi kulingana na luga yenye mshiriki anapenda (Kifaransa, Kinande, Kiswahili, Lingala). Washiriki wako kati ya miaka 18 na zaidi ya miaka 65. Tunataka kuzingatia maoni ya watu wenye kuwa katika mazingira magumu zaidi na ndiyo kwa maana washiriki wengi wako kati ya miaka 50 na zaidi ya miaka 65.

## Unafanya nini na habari yenye minakupatia? Unachangia hii matokeo na nani?

Majibu yako yote yenye utapana haitajulikana. Ni kusema kama hatuta ruhusu mtu mwingine kujua ma jibu yako. Ma jibu yako itachanganywa na ma jibu ya watu wengine watakao shiriki kwenye hii utafiti kwa ajili tuweze kuzungumuza juu ya kile kila mtu anasema kama kikundi. Habari zote zinazo kuhusu zitalindwa kwa siri na jina yako haitatajwa katika ripoti zetu zote au matokeo ya hii utafiti.

Matokeo ya hii utafiti zitagawanywa kwa mashirika (ONG) zingine (kwa mfano Mercy Corps) na hasa mashirika inayo fanya kazi katika sekta ya mawasiliano katika hali za hatari na ushiriki wa kijamii (CREC au RCCE mu kingereza). Haya ni mashirika ambazo zina shaba ya *«kuhimiza watu na jamii, na kuzungumuza nao kwa utaratibu kwa ajili ya kuwapa uwezo wa kujifunza tabia nzuri na kuzuwia kusambarana kwa magonjwa ya kuambukiza zinazo gusa watu ndani ya inchi»*.

TWB inaweza pia kutangaza hii matokeo katika mazungumuzo na washirika wake juu ya kuwasaidia kupanga mawasiliano ya siku zijazo kuhusu ugonjwa wa corona na mada zingine (kwa mfano, muundo (format) na luga yenye inapendwa kwa kupokea habari).

## Juu ya nini wachunguzi (enqueteurs) hawajibiake ma swali yetu moja kwa moja wakati wa mahojiano?

Siyo kila wakati njo tunaweza kutoa moja kwa moja ma jibu na habari kwa washiriki kwa sababu wachunguzi au shirika yetu hatuko madaktari au wataalamu katika ugonjwa wa corona. Kwa kutoa habari moja kwa moja kwa mshiriki, tuna hatari ya kutokuelewana. Ndiyo sababu tunagawa ma swali na watu wengine kwenye sekta ya mawasiliano au upashaji wa habari kwa ajili ya kuanda ma jibu inayo faa. Tutajaribu kuchangia na washiriki oroza (liste) ya vyanzo ya kuaminika ambazo zinatoa habari zaidi kuhusu ugonjwa wa corona na vinaweza kujibu ma swali yako.

## Ugonjwa wa corona siyo wasiwasi kubwa ndani ya jamii yetu. Kwa nini hamufanyi utafiti juu ya mada muhimu zaidi kwetu (kama usalama au magonjwa zingine hatari zaidi)?

TWB ni shirika ambayo inataka kuona dunia ambapo kila mtu anapokea habari katika luga na muundo (format) yenye anaelewa muzuri. Upashi wa habari kuhusu ugonjwa wa corona unaleta shida za kipekee - siyo tu kwamba ni ugonjwa mupya ambao hatuya elewa muzuri na ambao ulisumbua sana dunia, lakini pia ulileta hali ya habari mingi za uwongo. Ndiyo sababu tunazani kwamba ni muhimu kwetu kuelewa maoni ya watu kuhusu hii mada.

Pia, aina hii ya utafiti inatuwezesha kuelewa shida kuhusu upashaji wa habari (mawasiliano) ndani ya jamii wakati wa shida (kama vile miripuko ya magonjwa) na kisha kuwashauri washirika (partenaires) wetu gisi ya kuboresha hii mawasiliano kwa sasa na siku zijazo.

## Translators without Borders (Watafsiri wasiyo na Mipaka) ni nani?

Translators without Borders (TWB) ni shirika isiyo kuwa ya faida (ONG). Wakati wa shida, TWB inatoa musaada wa ki luga kwa mashirika zingine za kibinadamu duniani. Lengo ya TWB ni kusaidia katika mawasiliano kati ya jamii na mashirika ambazo zinataka kuzisaidia. Tunazani kwamba kila mtu iko na haki ya kupokea habari mu luga yenye anaelewa. Kama unataka kujua zaidi juu ya kazi yetu, unaweza kutembelea site internet yetu - <https://translatorswithoutborders.org>, lakini kwa sasa inapatikana tu mu luga ya kingereza. Tuko naianda ipatikane mu luga mingi zaidi.

## Vyanzo ili kupata habari zaidi kuhusu ugonjwa wa corona

### Kama unatumia mtandao wa internet

**Uji Chatbot kwenye WhatsApp:** +243 844 434 444

### Kama hautumii mtandao wa internet

**Radio ya Wizara (Ministere) ya Afya:** FM 95.7

**Coracon, kipindi "Tupone Wote"**

**Piga simu bila malipo kwenye moja kati ya hizi numeros tatu za telefone 101, 109 na 110.** Hizo ni numeros za telefone za kituo cha kupokea simu (centre d'appel) cha Wizara (Ministere) ya Afya pamoja na UNICEF.

**Viamo hotline santé** - kwenye numero 42502 (kwa kutumia Vodacom tu)

